JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**BUNGE LA TANZANIA**

KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ELIMU, UTAMADUNI NA MICHEZO

# TAARIFA KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027

*(Kwa mujibu wa Kanuni ya 121(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge za Mwaka 2025)*

**4 MEI, 2026**

## YALIYOMO

*Ukurasa*

**YALIYOMO** ..... i
**ORODHA YA MAJEDWALI** ..... ii
**ORODHA YA CHATI** ..... iii
**SEHEMU YA KWANZA** ..... 1
1.0 **UTANGULIZI** ..... 1
1.1 Maelezo ya Jumla ..... 1
1.2 Muundo wa Taarifa ..... 1
1.3 Msingi, Mbinu na Wigo wa Kazi ya Kamati ..... 2
1.3.1 Msingi ..... 2
1.3.2 Mbinu na Njia Zilizotumika ..... 3
1.3.3 Wigo wa Kazi ..... 4
1.4 Majumuisho ya Sehemu ..... 5
**SEHEMU YA PILI** ..... 6
2.0 **UCHAMBUZI WA UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA** 2025/2026 ..... 6
2.1 Maelezo ya Jumla ..... 6
2.2 Uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji ..... 6
2.2.1 Uzingatiaji wa Ushauri wa Kamati ..... 7
2.2.2 Ukusanyaji wa Maduhuli ..... 10
2.2.3 Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ..... 15
2.2.4 Utekelezaji wa Kazi Zilizopangwa ..... 16
2.2.5 Mwenendo wa Upatikanaji wa Fedha za Bajeti ..... 18
2.3 Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 ..... 20
2.3.1 Makadirio ya Mapato ..... 22
2.3.2 Makadirio ya Matumizi ya Maendeleo ..... 27
2.3.3 Makadirio ya Matumizi ya Kawaida ..... 28
2.4 Majumuisho ya Sehemu ya Pili ..... 29
**SEHEMU YA TATU** ..... 31
3.0 **MAONI, USHAURI NA HITIMISHO** ..... 31
3.1 Maoni ..... 31
3.2 Ushauri ..... 32
3.3 Hitimisho ..... 34
**VIAMBATISHO** ..... 37
**KIAMBATISHO NA 1** ..... 37
**KIAMBATISHO NA 2** ..... 43

## ORODHA YA MAJEDWALI

***Ukurasa***

**Jedwali Na. 1**: Ukusanyaji wa Maduhuli kwa Mwaka 2025/2026 - Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo ........................................................ 11

**Jedwali Na. 2:** Mwenendo wa Upatikanaji wa Fedha za Matumizi ya Kawaida na Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 ......................... 19

**Jedwali Na. 3:** Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa Mwaka 2025/2026 na Mwaka 2026/2027 ........................................................................ 23

**Jedwali Na. 4:** Ulinganisho wa Bajeti ya Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa Miradi ya Maendeleo, Mishahara na Matumizi Mengineyo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 na 2026/2027 ...... 28

# ORODHA YA CHATI

***Ukurasa***

**Chati Na. 1:** Ukusanyaji wa Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 - Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo ............................................. 11

**Chati Na. 2:** Mwenendo wa Upatikanaji wa Fedha za maumizi ya Kawaida na Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 ...................................... 20

**Chati Na. 3:** Ulinganisho wa Ukusanyaji wa Maduhuli Fungu 96 2025/2026 na 2026/2027 ............................................................................................. 23

**Chati Na. 4:** Ulinganisho wa Bajeti 2025/2026 na 2026/2027 (Fungu 96) ................. 28

## SEHEMU YA KWANZA

## 1.0 UTANGULIZI

### 1.1 Maelezo ya Jumla

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 121 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge za Mwaka 2025, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo (**Fungu 96**) kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027. Taarifa inayowasilishwa ni matokeo ya shughuli za Kamati kwa kipindi cha tarehe 09 hadi 27 Machi, 2026 kutokana na uchambuzi wa makadirio ya mapato na Matumizi ya Sekta zilizo chini ya Kamati hii.

### 1.2 Muundo wa Taarifa

**Mheshimiwa Spika,** sehemu hii inabainisha mtiririko wa maudhui pamoja na kuzingatia masharti ya Kanuni ya 145 ya Kanuni za Bunge, kuhusu muundo wa Taarifa yoyote ya Kamati inayowasilishwa Bungeni. Lengo ni kuliwezesha Bunge kufuatilia mtiririko wa taarifa na kuonesha taarifa inavyozingatia masharti ya Kanuni za Bunge kuhusu muundo wa Taarifa. Kwa maelezo hayo, Taarifa hii imegawanyika katika sehumu kuu tatu ambazo ni:

(i) Sehemu ya **Kwanza** inatoa maelezo ya jumla na kuonesha Msingi, Mbinu na Wigo wa Kazi ya Kamati katika kufanyia kazi makadirio ya mapato na Matumizi ya Wizara hii.

(ii) Sehemu ya **Pili** inabainisha matokeo ya uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti kwa Wizara hii kwa Mwaka wa fedha 2025/2026 na uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2026/2027.

(iii) Sehemu ya **Tatu** inabainisha Maoni na Ushauri wa Kamati na kumalizia kwa hitimisho.

## 1.3 Msingi, Mbinu na Wigo wa Kazi ya Kamati

### 1.3.1 Msingi

**Mheshimiwa Spika,** msingi wa Kamati kuchambua taarifa ya Utekelezaji na Makadirio ya Bajeti ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo **(Fungu 96)** ni masharti ya Kanuni za Kudumu za Bunge za Mwaka 2025. Kifungu cha 5 (7) (g) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge, kikisomwa kwa pamoja na Kifungu cha 7 (1) (a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge, kinaipa Kamati hii jukumu la kushughulikia Bajeti ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo. Aidha, Kanuni ya 120 (2) ya Kanuni za Bunge ilitaka makadirio haya yajadiliwe na Kamati kabla ya kuwasilishwa Bungeni leo. Naomba kulihakikishia Bunge hili kuwa masharti hayo yalitimizwa.

**Mheshimiwa Spika**, mapema asubuhi ya leo, taarifa hii iliwekwa mezani kwa mujibu wa Kanuni ya 121 (5) ya Kanuni za Bunge. Na sasa, nawasilisha taarifa hii kwa mujibu wa Kanuni ya 121 (9) ya Kanuni za Bunge kama nilivyoeleza hapo awali.

### 1.3.2 Mbinu na Njia Zilizotumika

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebainisha njia zilizotumika kufanyia kazi hoja hii kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 145 (a) (iii) ya Kanuni za Bunge. Lengo ni kuiwezesha Taarifa hii kuwa rejea madhubuti, inayosaidia mjadala wa Bunge kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara. Kwa kufanya hivyo, Kamati inajenga msingi wa uadilifu uliozingatiwa ili kupata maoni na ushauri wake.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilitumia mbinu mbalimbali za uchambuzi zikiwemo kupokea maelezo ya Waziri, kuhoji mambo yaliyojitokeza na kupokea majibu ya mtoa hoja. Uchambuzi wa majibu na mawasilisho ulifanyika kwa kufanya ulinganisho kimaudhui na uhalisia. Haya yote yamefanikisha kupatikana kwa taarifa hii ambayo inabainisha maoni na ushauri wa kufanyiwa kazi katika hoja hii inayohusu makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo.

### 1.3.3 Wigo wa Kazi

**Mheshimiwa Spika,** madhumuni ya Taarifa hii ni kulipatia Bunge tathmini ya Kibunge kwa misingi ya ushahidi kuhusu makadirio ya matumizi na mapato yaliyowasilishwa na Mtoa hoja. Lengo ni kuongoza mjadala unaozingatia uwajibikaji wa kibajeti na kuhakikisha kuwa rasilimali za umma zinatengwa kwa kuzingatia vipaumbele vya kitaifa na Ilani ya Chama Cha Mapinduzi ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025 inayoeleza; **nanukuu:**

> *"Utamaduni, sanaa na michezo ni sekta muhimu katika kuchochea ukuaji wa uchumi endelevu kwa kuzalisha fursa za ajira, kuchochea mauzo ya bidhaa za kitamaduni ndani na nje ya nchi, kuvutia uwekezaji, kukuza utalii na kuitangaza nchi kimataifa."* (uk. 35). **Mwisho wa kunukuu.**

**Mheshimiwa Spika**, kimsingi Taarifa hii inagusa utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2025/2026 na Makadirio ya bajeti kwa mwaka wa fedha 2026/2027. Maudhui yake yanahusu utekelezaji wa miradi ya maendeleo, ukusanyaji wa maduhuli, upatikanaji wa fedha na uzingatiaji wa ushauri uliotolewa na Kamati wakati Bunge lilipopitisha bajeti ya Wizara hii. Eneo lingine la maudhui ya Taarifa hii linagusa makadirio ya ukusanyaji wa maduhuli, ulinganisho wa vipaumbele na bajeti inayoombwa kwa mwaka wa fedha 2026/2027.

## 1.4 Majumuisho ya Sehemu

**Mheshimiwa Spika,** kwa ujumla sehemu ya Kwanza inaonesha ombi la kuiwasilisha rasmi Taarifa hii katika majadiliano ya Bunge, muundo unavyozingatia masharti ya Kanuni ya 145 ya Kanuni za Bunge na kubainisha msingi wa Kamati kufanyia kazi makadirio ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo. Maelezo haya yamewekwa kwa muktadha na msingi wa maudhui ya Taarifa. Kwa kufanya hivyo, sehemu hiyo inalisaidia Bunge kuona nmna taarifa ilivyozingatia taratibu za Kibunge ikiwemo dhana ya uchunguzi wa Kibunge kuzingatia Ushahidi *(Evidence based scrutiny)*.

## SEHEMU YA PILI

## 2.0 UCHAMBUZI WA UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026

### 2.1 Maelezo ya Jumla

**Mheshimwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, sehemu ya pili ya Taarifa hii inatoa maelezo kamili kuhusu mambo yote yaliyochambuliwa na Kamati. Sehemu hii itakuwa na maelezo kuhusu mambo makuu mawili. Mambo hayo ni: -

(i) Uchambuzi wa Taarifa ya utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026; na

(ii) Uchambuzi wa makadirio ya mapato na matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi huo ulifanyika kwa ulinganisho kama ilivyoelekeza Kanuni ya 120 (1) na (2) za Kanuni za Bunge. Ni uchambuzi unaojenga msingi wa maoni na ushauri wa Kamati.

### 2.2 Uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji

**Mheshimiwa Spika**, ili kukidhi masharti ya Kanuni za Bunge, tarehe 26 Machi, 2026, Kamati ilipokea taarifa ya utekelezaji wa Bajeti ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2025/2026 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2026/2027. Lengo lilikuwa ni kuliwezesha Bunge kulinganisha

dhamira yake wakati wa kupitisha bajeti na matokeo. Aidha, uchambuzi wa makadirio ya bajeti kwa mwaka wa fedha 2026/2027 ulilenga kuliwezesha Bunge kupitisha bajeti ya Wizara hii kwa namna yenye mchango unaolingana na ahadi waliyopewa wananchi kupitia Ilani ya CCM iliyorejewa.

**Mheshimiwa Spika**, kwa madhumuni hayo, sehemu hii inatoa matokeo ya uchambuzi wa mambo matano ambayo ni:

(i) Uzingatiaji wa Ushauri wa Kamati;

(ii) Utekelezaji wa Kazi zilizopangwa;

(iii) Ukusanyaji wa Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026;

(iv) Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo; na

(v) Mwenendo wa Upatikanaji wa Fedha za Bajeti.

### 2.2.1 Uzingatiaji wa Ushauri wa Kamati

**Mheshimiwa Spika**, sehemu hii ya Taarifa inatoa mrejesho na fursa kwa Bunge na Umma kufahamu kiwango cha Serikali kuzingatia ushauri uliotolewa Bungeni kuhusu matumizi ya rasilimali za umma. Kwa kufanya hivyo, taarifa hii inapima dhamira ya Serikali katika kutekeleza vipaumbele vilivyoainishwa kwa ufanisi uliokusudiwa na Bunge kukidhi matarajio ya wananchi.

**Mheshimiwa Spika**, wakati wa uchambuzi wa Bajeti ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa Mwaka wa

Fedha 2025/2026, Kamati ilitoa maoni na ushauri kuhusu mambo mbalimbali kwa lengo la kuboresha utekelezaji wa majukumu ya Wizara hii. Naomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba kwa sehemu kubwa ushauri wa Kamati ulizingatiwa na sehemu nyingine, utekelezaji wake ni endelevu kama inavyobainishwa katika **Kiambatisho Na. 2.**

**Mheshimiwa Spika,** mfano wa ushauri uliozingatiwa unahusu jukumu la Serikali kuendelea kutenga bajeti kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa Uwanja wa Arusha. Ushauri huu ulilenga kufanikisha na kukamilisha utekelezaji wa mradi huu kama ilivyokusudiwa na pia kuongeza chachu ya utalii na kuwa kituo muhimu katika Mashindano ya Mataifa ya Afrika (AFCON).

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa iliyotolewa kwenye Kamati inaonesha kwamba katika mwaka wa fedha 2024/2025, Serikali ilitenga na kutoa kiasi cha **shilingi 153,161,763,553.50** kwa ajili ya ujenzi wa uwanja wa Arusha. Ili kuhakikisha inakamilisha maandalizi ya kuwa mwenyeji wa mashindano ya AFCON 2027, kwa kushirikiana na nchi za Kenya na Uganda, kwa mwaka wa fedha 2025/2026, imetenga jumla ya **shilingi 162,976,682,000.00** kwa ajili ya mradi wa ujenzi wa uwanja wa Arusha. Hadi Februari 2026, Serikali imetoa jumla ya **shilingi 106,742,579,088** sawa na **asilimia 65.5** ya bajeti iliyotengwa. Aidha, hadi Februari 2026 ujenzi wa uwanja umefikia **asilimia 75** na jumla ya **shilingi 256,208,264,022.55** zimetolewa, sawa na **asilimia 73.8** ya gharama ya mradi. Hata hivyo, katika mwaka

wa fedha 2026/2027 Wizara imeendelea kutenga bajeti kwa ajili ya Ujenzi wa eneo Changamani la Michezo Arusha kiasi cha **shilingi 125,653,212,000.**

**Mheshimiwa Spika,** Vilevile ushauri wa kuandaa mikakati ya kuboresha viwanja vingine vyenye hadhi ya kuendesha mashindano ya kitaifa na kimataifa ili kupunguza mfululizo wa matumizi ya Uwanja wa Benjamin Mkapa ulizingatiwa ambapo serikali imeendelea na ukarabati na ujenzi wa viwanja vipya vya michezo.

**Mheshimiwa Spika,** mfano wa viwanja hivyo vilivyokarabatiwa ili kukidhi vigezo ni uwanja wa Uhuru, Meja Jenerali Isamuhyo, Gymkana na uwanja wa shule ya Sheria (Law school). Vile vile, Serikali imeanza ujenzi wa viwanja vitatu (3) vya Farasi, Gymkana Annex na Leaders Club. Katika hatua nyingine, Serikali inajenga viwanja vitano (5) vya mazoezi jijini Arusha katika eneo la Magereza, Kisongo, Uwanja wa Mgambo, eneo la Police Field Force na Engutoto. Viwanja hivi vitatumika wakati wa Mashindano ya Mpira wa Miguu kwa timu za Taifa za Wanaume Afrika (AFCON 2027).

**Mheshimiwa Spika**, upo pia ushauri wa Kamati ambao uzingatiaji wake haujakamilika. Ushauri huo ulihusu yafuatayo:-

(a) Kuongeza wigo wa ukusanyaji wa Mapato ya Tozo za Hakimiliki kwa kuongeza vifaa vinavyotozwa Tozo hii hasa vya Kidijitali;

(b) Fedha kwa ajili ya ujenzi na ununuzi wa mitambo ya uchapaji kutolewa kabla ya tarehe 01 Julai, 2025; na

(c) Ujenzi wa Jengo la Kiwanda cha Uchapishaji ili kupunguza gharama za uendeshaji na utunzaji wa mitambo katika maghala ya Taasisi nyingine.

**Mheshimiwa Spika,** ushauri wa Kamati ulijengwa kwa misingi halisi inayostahili kupewa uzito wake. Kamati ina maoni kwamba, kutokuzingatia ushauri wake ni jambo linaloweza kutatiza azma ya kutimiza matarajio ya wananchi. Aidha, mtiririko wa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ulichangia kutozingatiwa ipasavyo kwa baadhi ya ushauri uliotolewa.

### 2.2.2 Ukusanyaji wa Maduhuli

**Mheshimiwa Spika**, lengo la uchambuzi wa taarifa za makusanyo ya maduhuli kwa Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo ni kuliwezesha Bunge kubaini iwapo lengo la makusanyo lililoidhinishwa na Bunge limefikiwa. Hata hivyo, uchambuzi huu unaliweka Bunge katika nafasi ya kutoa uzoefu unaopatikana kwa mwaka wa fedha 2025/2026 na kubaini uhalisia unavyostahili kwa mwaka wa fedha 2026/2027. Kamati ilifanya uchambuzi kwa kuzingatia masuala yafuatayo:-

(i) Kiasi kilichokusanywa ikilinganishwa na lengo la makusanyo; na

(ii) Ulinganisho wa kipindi kama hicho kwa mwaka wa fedha 2025/2026

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2025/2026, Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo ililenga kukusanya maduhuli ya jumla ya **Shilingi 41,331,192,000.** Hadi kufikia Mwezi Februari 2026, Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo ilikuwa imekusanya **Shilingi 14,656,583,088.86** sawa na asilimia **35.46** ya malengo yaliyokusudiwa. Mchanganuo wa fedha hizo ni kama inavyoonekana katika Jedwali Na 1.


**Jedwali Na 1: Ukusanyaji wa Maduhuli kwa Mwaka 2025/2026 - Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo**

| UKUSANYAJI WA MADUHULI FUNGU 96 KWA MWAKA 2025/2026 | | | |
|---|---|---|---|
| **CHANZO** | **MAKADIRIO** | **MAKUSANYO** | **ASILIMIA** |
| Idara na Vitengo Wizarani | 1,036,000,000 | 661,373,423 | **63.8** |
| Taasisi | 40,295,192,000 | 13,995,209,665.86 | **34.7** |
| **JUMLA** | **41,331,192,000** | **14,656,583,088.86** | **35.46** |

**Chanzo:** *Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kuhusu Mwelekeo wa Bajeti kwa Mwaka 2025/2026*

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa data kwenye jedwali hilo, unabainika katika chati duara *(pie chart)* ili kurahisisha ulinganisho uliokusudiwa kwenye Kanuni ya 120 (2) ya Kanuni za Bunge. Picha halisi ya uchambuzi huo inaonekana katika Chati Na. 1

**Chati Na. 1: Ukusanyaji wa Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 - Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo**




**Chanzo:** *Usanifu wa Kamati kutoka kwenye Jedwali Na, 1 la Taarifa hii*

**Mheshimiwa Spika,** taswira iliyojitokeza inaonesha kwamba:

(i) Mwenendo wa Jumla wa makusanyo hadi kufikia Mwezi Februari, 2026 ni **asilimia 35.46** ambayo ni pungufu ya nusu ilihali kipindi cha utekelezaji kimevuka nusu mwaka;

(ii) Uwiano wa makusanyo kwa lengo umekuwa hafifu zaidi katika Taasisi zilizo chini ya Wizara kuliko Idara na Vitengo vilivyoko Wizarani. Wakati Idara na Vitengo vya Wizara vimefikia **asilimia 63.8** ya lengo, Taasisi zimefikia **asilimia 34.7** ya lengo.

(iii) Kwa ujumla mwenendo wa makusanyo kwa baadhi ya taasisi ni hafifu zaidi. Mathalani Bodi ya Filamu

Tanzania imekusanya **asilimia 27** ya lengo la makusanyo yake.

**Mheshimiwa Spika,** kwa ujumla Kamati imebaini kwamba uwiano wa lengo la makusanyo kati ya Wizara na taasisi zake ulitofautiana na uwiano wa makusanyo halisi kati ya Wizara na taasisi. Ufafanuzi umeonesha kwamba, wakati wa makadirio ya Wizara ilitarajiwa kukusanya **asilimia 2.50** ya lengo la makusanyo ya Wizara na taasisi zake. Katika utekelezaji Wizara imekusanya **asilimia 4.51** ya jumla ya makusanyo ya Wizara na taasisi zake.

**Mheshimiwa Spika,** kwa uwiano huo, lengo la makusanyo kwenye taasisi za Wizara linahitaji kuangaliwa vizuri. Aidha, utaratibu na utekelezaji wa makusanyo kwa ujumla unahitaji kufanyiwa tathmini ipasavyo.

**Mheshimiwa Spika**, matokeo ya uchambuzi huu yameweka bayana kuwa kuna uwezekano mdogo sana wa kufikia lengo la makusanyo ambapo kunaweza kuathiri utekelezaji wa Bajeti Kuu ya Serikali kwa kuwa makusanyo hayo ni sehemu ya mapato yaliyozingatiwa katika bajeti ya matumizi kwa mwaka wa fedha 2025/2026.

**Mheshimiwa Spika,** mwenendo kwa ujumla wa makusanyo katika baadhi ya taasisi zilizo chini ya Wizara hii hauoneshi

uwezekano wa kukamilika kwa lengo. Mathalani, makusanyo kwa Bodi ya Filamu Tanzania hadi kufikia mwezi Februari, 2026 ni **asilimia 27** tu. Hali hii ni ishara kuwa makusanyo ya jumla ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2025/2026 yanaweza yasifikie malengo ifikapo tarehe 30 Juni, 2026.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilihoji sababu za makusanyo duni ya maduhuli kwa baadhi ya taasisi na kuchangia pengo la ufikiaji wa lengo. Kamati ilijulishwa kwamba, kupungua kwa idadi ya waandaaji wa filamu kutokana na mabadiliko ya soko la filamu pamoja na kukua kwa teknolojia kumesababisha waandaaji wengi kuandaa na kurusha filamu kupitia program tumizi (App) kwa kutumia vifaa rahisi zikiwemo simu janja kunasababisha wengi kutokufuata taratibu zilizowekwa na Serikali na hivyo kumeikosesha Bodi ya Filamu Tanzania mapato yaliyolengwa.

**Mheshimiwa Spika**, sababu nyingine ni Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA) kuondolewa kwa baadhi ya vyanzo vya mapato ambavyo vilikuwa na mchango mkubwa kwenye makusanyo kama vile Ada za kumbi za starehe na burudani pamoja na Ada za matukio ya kazi za Sanaa ambazo zilikuwa zimekadiriwa kukusanywa shilingi **755,000,000**.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na sababu hizo ni ukweli usiopingika kwamba mabadiliko ya Teknolojia ni jambo lisiloepukika katika sekta ya habari, sekta ya sanaa, sekta ya michezo na sekta ya utamaduni jambo linalohitaji kuendana

na maendeleo ya dunia, kurahisisha mawasiliano, kuboresha ubunifu na kuongeza ufanisi katika uzalishaji na usambazaji wa taarifa na kazi za kisanii.

### 2.2.3 Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 120(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ilifanya ziara katika Mikoa ya Arusha na Dar es Salaam. Kamati ilikagua miradi mitatu ambayo ni sehemu ya miradi iliyotengewa fedha kwa mwaka 2025/2026. Naomba kubainisha kuwa Kamati ilipokea taarifa ya upatikanaji wa fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo na kuchambua utekelezaji wa miradi hiyo. Ufafanuzi zaidi kuhusu Miradi unaambatishwa pamoja na Taarifa hii **(Kiambatisho Na1).**

**Mheshimiwa Spika,** matokeo ya jumla ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo yanaonesha kama ifuatavyo:

(i) Kiasi cha fedha kilichopokelewa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya Maendeleo ni **asilimia 63.2** ya bajeti yote.

(ii) Kwa ujumla, upatikanaji wa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mitatu iliyokaguliwa umefikia wastani wa **asilimia 72.89**

(iii) Mwenendo wa Utekelezaji wa miradi hiyo unaendana na upatikanaji wa fedha. Hata hivyo, Utekelezaji wa **Mradi Na. 6505**, Ujenzi na Ununuzi wa Mitambo ya Uchapaji wa Magazeti ya Serikali hauendelei kwa kasi iliyokusudiwa.

### 2.2.4 Utekelezaji wa Kazi Zilizopangwa

**Mheshimiwa Spika,** tarehe 26 Machi, 2026 Kamati ilipokea na kuchambua Taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026. Wakati wa uchambuzi Kamati ilizingatia vipaumbele vya Wizara na kufanya tathmini ya hali halisi ya utekelezaji wa kazi zilizopangwa ikilinganishwa na Bajeti iliyopitishwa na Bunge. Uchambuzi ulionesha kuwa mipango na majukumu yaliendana na upatikanaji wa fedha kwa mwaka unaohusika.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi ulionesha kuwa majukumu na mipango ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2025/2026 yapo katika hatua nzuri za utekelezaji. Kwa mfano, Wizara ilikuwa imepanga kuratibu maandalizi ya Michuano ya CHAN 2024 na AFCON 2027. Serikali ilieleza kwamba katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Februari, 2026 Wizara imeratibu maandalizi ya mashindano ya Mpira wa Miguu Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN 2024) kwa mafanikio makubwa. Mashindano haya yalifanyika kuanzia 02 hadi 30 Agosti, 2025 kwa kushirikiana na nchi za Kenya na Uganda.

**Mheshimiwa Spika,** Timu ya Taifa ya Tanzania (Taifa Stars) ilishiriki katika mashindano haya kwa mara ya tatu na kupata mafanikio makubwa ambapo ilifika hatua ya robo fainali. Tanzania ilipokea tuzo ya heshima kutoka Shirikisho la Mpira wa

Miguu Barani Afrika (CAF) kwa kufanya vizuri katika maandalizi na uratibu wa mashindano hayo.

**Mheshimiwa Spika,** vilevile Wizara imeendelea na maandalizi ya Mashindano ya Mpira wa Miguu kwa timu za Taifa za Wanaume Afrika (AFCON 2027) kwa kutekeleza majukumu mbalimbali hususan ujenzi na ukarabati wa miundombinu itakayotumika katika mashindano hayo ikiwemo ukarabati wa Uwanja wa Benjamin Mkapa ambao umefikia asilimia **95**, ukarabati wa Uwanja wa Uhuru ambao umefikia asilimia **70**, na viwanja vya mazoezi vya Uwanja wa Gymkhana, Meja Jenerali Isamuhyo na Shule ya Sheria vimekamilika.

**Mheshimiwa Spika,** ujenzi wa viwanja vingine vya mazoezi kwa ajili ya AFCON 2027 ambavyo ni Farasi, Leaders Club na Gymkhana 2 vya Jijini Dar es Salaam vipo katika hatua za awali za ujenzi ambapo mkandarasi amekabidhiwa eneo. Vilevile, katika Jiji la Arusha, Wizara inaendelea kusimamia ujenzi wa Uwanja mkubwa wa michezo utakaokuwa na uwezo wa kubeba mashabiki 32,000 ambao umefikia asilimia **75.** Kwa upande wa viwanja vya mazoezi Wizara imeainisha maeneo ya Mgambo, Magereza, Kisongo na Engutoto.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilijulishwa zaidi kuhusu mikakati ya kupeleka Kiswahili Kimataifa kwa kufungua vituo vya Kufundisha Kiswahili kwa wageni katika nchi 10. Serikali ilieleza kwamba katika kuendeleza na kueneza Kiswahili Kimataifa

jumla ya vituo vitatu (3) katika nchi mbili (2) vilifunguliwa kwa kushirikiana na Ubalozi wa Tanzania nchini Afrika Kusini ambapo imesajili vituo viwili (2) vya kufundishia Kiswahili kwa wageni katika Jiji la Johannesburg. Vituo hivyo ni Kiswahili Centre of Excellence South Africa (KCESA) na Tanzania Kiswahili Cultural Centre ambavyo vinamilikiwa na Watanzania waishio Afrika Kusini. Aidha, kituo kimoja cha Imani Languages Academy kinachomilikiwa na Mtanzania kimesajiliwa nchini Japan.

### 2.2.5 Mwenendo wa Upatikanaji wa Fedha za Bajeti

**Mheshimiwa Spika,** ufanisi wa utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo unategemea mwenendo wa upatikanaji wa fedha kutoka Hazina kama ilivyoidhinishwa na Bunge lako Tukufu. Kwa kuzingatia hilo, Kamati ilipokea na kuchambua mwenendo wa upatikanaji wa fedha kwa **Fungu 96** kama ilivyoelezwa na mtoa hoja. Kwa mwaka wa Fedha 2025/2026, Wizara hii iliidhinishiwa jumla ya **shilingi 61,469,285,000** sawa na **asilimia 11.82** kwa ajili ya matumizi ya Kawaida na jumla ya **shilingi 458,190,778,000** sawa na **asilimia 88.17** kwa ajili ya matumizi ya Miradi ya Maendeleo. Uchambuzi ulibainisha yafuatayo:

(i) Kiasi cha fedha kilichoidhinishwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida ya Wizara hii asilimia **11.82** ya Bajeti yote ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2025/2026 ililenga matumizi

ya kawaida, lakini fedha iliyopatikana kwa ajili ya matumizi ya kawaida ni asilimia **11.70**. Uwiano huo hautofautiani na mtazamo uliokuwepo wakati wa kupitisha bajeti.

(ii) Kiasi cha bajeti ya matumizi ya kawaida kilichotengwa kwa matumizi mengineyo ni asilimia **45.6,** lakini kiasi cha fedha za matumizi ya kawaida kilichopatikana kwa ajili ya matumizi mengineyo ni asilimia **43.14** ya bajeti ya matumizi ya kawaida. Uwiano huu hautofautiani sana.

(iii) Kati ya fedha hizo **Shilingi 28,065,472,000** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo, **Shilingi 33,403,813,000** ni kwa ajili ya mishahara na **Shilingi 458,190,778,000** kwa ajili ya miradi ya maendeleo.


**Mheshimiwa Spika,** Mwenendo huo wa upatikanaji wa fedha unaonekana katika **Jedwali Na.2**

**Jedwali Na. 2: Mwenendo wa Upatikanaji wa Fedha za Matumizi ya Kawaida na Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026**

| **UPATIKANAJI WA FEDHA FUNGU 96 MWAKA 2025/2026** | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **MATUMIZI** | | **KILICHOIDHINISHWA** | **KILICHOPOKELEWA** | **ASILIMIA** |
| **KAWAIDA** | MISHAHARA | 33,403,813,000 | 21,852,172,806.12 | **65.4** |
| | OC | 28,065,472,000 | 16,583,499,387.28 | **59.1** |
| **MAENDELEO** | NDANI | 458,190,778,000 | 289,878,498,984.34 | **63.3** |
| **JUMLA BAJETI** | | **519,660,073,000** | **328,314,171,177.74** | **63.2** |

**Chanzo:** *Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kuhusu Mwelekeo wa Bajeti kwa Mwaka 2025/2026*

**Chati Na. 2: Mwenendo wa Upatikanaji wa Fedha za matumizi ya Kawaida na Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026**




**Chanzo:** *Usanifu wa Kamati kutoka kwenye Taarifa za Randama ya Wizara kwa Mwaka 2025/2026*

## 2.3 Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027

**Mheshimiwa Spika**, ili kuzingatia masharti ya Kanuni ya 120 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ilichambua na kujadili Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa kuzingatia kazi zilizopangwa kutekelezwa kwa mwaka wa fedha 2026/2027. Wakati wa uchambuzi, Kamati ilijielekeza katika maeneo yafuatayo:-

(i) Makadirio ya ukusanyaji wa Maduhuli;

(ii) Makadirio ya Mapato kwa mwaka wa fedha 2026/2027; na

(iii) Makadirio ya Matumizi kwa mwaka wa fedha 2026/2027.

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa maeneo hayo ulifanyika kwa kuzingatia mipango na majukumu ya msingi ya Wizara hii na hotuba ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan aliyoitoa Bungeni tarehe 14 Novemba, 2025. Vilevile, uchambuzi ulizingatia mwelekeo wa Jumla wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050, ambapo imeeleza malengo mahususi katika Sekta ya Habari, Sekta ya Utamaduni na Sekta ya Sanaa na Michezo kama ifuatavyo:

(i) *"Kuwa na sekta ya habari inayofanya kazi kwa uhuru, uwazi na inayochochea uwajibikaji, uhuru wa kujieleza na upatikanaji sawa wa taarifa kama mhimili wa demokrasia hai. Aidha, katika muktadha huu, vyombo vya habari huru na vinavyojitegemea ni nyenzo muhimu katika kuhakikisha utawala bora na uwajibikaji; (uk.16)*

(ii) *Kutumia urithi wake wa kiutamaduni wenye utajiri mkubwa, sekta ya sanaa, ubunifu na michezo inayokua kwa kasi pamoja na Kiswahili kama nyenzo ya diplomasia na lugha yenye manufaa ya kiuchumi inayopanuka na kutambulika kimataifa. Hata hivyo, utamaduni utaongeza ushawishi wa Tanzania kupitia nyanja mbalimbali kwa kukuza Kiswahili kama nyenzo ya kidiplomasia na lugha yenye manufaa ya kiuchumi katika ushirikiano wa uwili, kikanda na kimataifa; (uk.28) na*

(iii) *Tanzania inalenga kuwa kitovu cha utamaduni, sanaa bunifu na michezo barani Afrika ifikapo mwaka 2050, ikiwa na sekta zinazostawi katika muziki, filamu,*

*mitindo, na burudani. Kwa kukuza vipaji na kuweka mazingira wezeshi, Tanzania itafungua milango ya ubunifu na ujasiriamali kwa vijana." (uk.61)* **mwisho wa kunukuu.**

**Mheshimiwa Spika,** misingi hiyo ya uchambuzi imezingatiwa kwa sababu inatoa mwelekeo rasmi wa sera, vipaumbele, na malengo ya maendeleo ya Taifa kwa kila sekta. Kwa sababu hiyo, mgawanyo na matumizi ya fedha za umma unaongozwa na ahadi, mipango na vipaumbele ambavyo Bunge linapaswa kujielekeza.

### 2.3.1 Makadirio ya Mapato


**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipokea taarifa kuhusu lengo la ukusanyaji wa maduhuli kwa mwaka wa fedha 2026/2027. Uchambuzi ulijikita zaidi katika lengo lililokuwa limewekwa kwa mwaka wa fedha 2025/2026. Aidha, katika mwaka wa fedha 2026/2027 Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo **Fungu 96** inakadiriwa kukusanya maduhuli jumla ya **Shilingi 41,956,692,000.** Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa makadirio haya yameongezeka kwa shilingi **625,500,000** sawa na asilimia **1.51** ikilinganishwa na makadirio ya makusanyo kwa mwaka wa fedha 2025/2026. Uchanganuzi wa makadirio hayo unaonekana katika **Jedwali Na. 3** na **Chati Na. 3**.

**Jedwali Na. 3: Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa Mwaka 2025/2026 na Mwaka 2026/2027**

| ULINGANISHO WA UKUSANYAJI WA MADUHULI (FUNGU 96) 2025/2026 NA 2026/2027 | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **CHANZO** | **2025/2026** | **2026/2027** | **ONGEZEKO/U PUNGUFU** | **% YA ONGEZEKO /UPUNGUFU** |
| **Idara na Vitengo Wizarani** | 1,036,000,000 | 1,058,000,000 | 22,000,000 | 2.1 |
| **Taasisi** | 40,295,192,000 | 40,898,692,000 | 603,500,000 | 1.5 |
| **JUMLA** | **41,331,192,000** | **41,956,692,000** | **625,500,000** | **1.51** |

**Chanzo:** *Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kuhusu Mwelekeo wa Bajeti kwa Mwaka 2026/2027*

**Chati Na. 3: Ulinganisho wa Ukusanyaji wa Maduhuli Fungu 96 2025/2026 na 2026/2027**




**Chanzo:** Usanifu wa Kamati kutoka kwenye Taarifa za Randama ya Wizara kwa Mwaka 2026/2027

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa makadirio hayo umeonesha kama ifuatavyo:-

(i) Makadirio ya makusanyo chini ya Wizara na taasisi zake kwa mwaka wa fedha 2026/2027, yameongezeka kwa **asilimia 1.51** ikilinganishwa na lengo la makusanyo kwa mwaka wa fedha 2025/2026;

(ii) Makadirio ya Makusanyo kwa Idara na Vitengo vya Wizara kwa mwaka wa fedha 2026/2027 yameongezeka kwa **asilimia 2.1** ikilinganishwa na makadirio hayo kwa mwaka wa fedha 2025/2026; na

(iii) Makadirio ya makusanyo kwa taasisi zilizo chini ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2026/2027 yameongezeka kwa **asilimia 1.5.**

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa makadirio ya mapato kwa mwaka wa fedha 2026/2027 ulilinganishwa na utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2025/2026 kwa lengo la kuzingatia uzoefu uliopatikana. Uchambuzi umeonesha mambo yafuatayo:-

(i) Ongezeko la **asilimia 1.51** katika makadirio ya mapato haliendani na uzoefu unaojitokeza katika Taarifa ya utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa fedha 2025/2026. Kwa uzoefu uliopita, hadi kufikia zaidi ya nusu ya kipindi cha utekelezaji, ukusanyaji ulikuwa chini kwa **asilimia 35.46,** jambo lililoashiria kuwa lengo halina mwelekeo wa kutimia. Hali hii

inaonesha kwamba lengo linalowekwa kwa mwaka wa fedha 2026/2027 linastahili kupungua badala ya kuongezeka.

(ii) Ongezeko la **asilimia 2.1** la makusanyo kwa Idara na Vitengo vya Wizara katika mwaka wa fedha 2026/2027 ni halisi kwani lina uwezekano wa kufikiwa.

(iii) Ongezeko la **asilimia 1.5** katika makadirio ya mapato kwa taasisi zilizo chini ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2026/2027, haliendani na uzoefu uliopatikana wakati wa utekelezaji kwa mwaka wa fedha 2025/2026. Taarifa ya utekelezaji ilionesha kwamba, hadi kufikia mwezi Februari, 2026, ukusanyaji wa mapato ya taasisi ulifikia **asilimia 34.7** ya lengo, kiwango ambacho kinaashiria kuwa hakitomudu ongezeko la makadirio linalopendekezwa.

(iv) Uwiano wa makadirio ya mapato kati ya Wizara na taasisi zake kwa mwaka wa fedha 2026/2027, hauendani na uwiano uliopatikana wakati wa utekelezaji wa bajeti kwa mwaka 2025/2026. Taarifa ya utekelezaji ilionesha kuwa katika ukusanyaji, Taasisi zilikusanya **asilimia 34.7** ya makusanyo yote na Wizara ilikusanya **asilimia 63.8** ya makusanyo yote. Makadirio kwa mwaka 2026/2027 yanaonesha

kuwa makadirio ya mapato ya taasisi ni **asilimia 97.47** ya jumla ya makadirio yote kwa **Fungu 96**.

**Mheshimiwa Spika,** mantiki ya Kanuni ya 120 (2) ya Kanuni za Bunge ni kuliwezesha Bunge kutumia uzoefu uliopatikana wakati wa utekelezaji ili kujadili bajeti kwa mwaka wa fedha unaofuata. Uzoefu uliopatikana kwa mwaka wa fedha 2025/2026 unaonesha kuwa uwiano wa uwezo wa Wizara katika makusanyo na taasisi zake ni **asilimia 63.8** kwa Wizara na **asilimia 34.7** kwa taasisi zake. Makadirio yasiyozingatia uwiano huo yanaashiria kupatikana kwa vyanzo vipya vya mapato kwenye taasisi zilizo chini ya Wizara hii.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi zaidi wa Kamati umeonesha kuwa karibu vyanzo vyote vya mapato kwa mwaka wa fedha ulioisha ndivyo vinavyoendelea kwa mwaka wa fedha 2026/2027. Tafsiri ya matokeo hayo inaashiria kuhitajika kwa tathmini ya lengo la mapato kwa **Fungu 96.** Kamati ina maoni kwamba, pamoja na kuwepo kwa ongezeko la ukusanyaji wa maduhuli, Wizara inahitaji kuongeza ubunifu katika kuibua vyanzo vipya vya mapato.

### 2.3.2 Makadirio ya Matumizi ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilichambua makadirio ya jumla ya **Shilingi 458,190,788,000** kwa ajili ya kugharamia Miradi ya Maendeleo inayopangwa kutekelezwa na Wizara kwa mwaka wa fedha 2026/2027. Uchambuzi huo umefanyika kwa ulinganisho na mwaka wa fedha wa 2025/2026. Matokeo ya uchambuzi yameonesha kuwa:-

(i) Makadirio ya bajeti hii ya miradi ya maendeleo hayajaongezeka kwa mwaka 2026/2027 ikilinganishwa na mwaka 2025/2026. Kamati imebaini kuwa Wizara hii haina miradi mipya na ratiba ya utekelezaji wa miradi ya awali haiongezi bajeti ya maendeleo.

(ii) Kwa ujumla Bajeti ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo imeongezeka kwa **asilimia 1.09** bila ongezeko lolote katika bajeti ya miradi ya maendeleo. Kwa takwimu hizi uendeshaji wa Wizara umeongezewa bajeti kiasi na miradi ya maendeleo itaendelea kama ilivyokuwa.


**Mheshimiwa Spika**, Kamati ina maoni kuwa, kuendelea kutenga fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo kutasaidia kukamilisha ujenzi wa miundombinu bora ya michezo Tanzania. Aidha, Kamati imefanya ulinganisho wa Bajeti ya miradi ya maendeleo, mishahara na matumizi mengineyo chini ya Wizara hii kwa Mwaka 2025/2026 na 2026/2027. Uchambuzi huo unaonekana katika **Jedwali Na. 4 na Chati Na. 4.**

**Jedwali Na. 4: Ulinganisho wa Bajeti ya Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa Miradi ya Maendeleo, Mishahara na Matumizi Mengineyo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 na 2026/2027**

| ULINGANISHO WA BAJETI 2025/2026 NA 2026/2027 (FUNGU 96) | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | MATUMIZI | 2025/2026 | 2026/2027 | ONGEZEKO/UPUNGUFU | % YA ONGEZEKO /UPUNGUFU |
| KAWAIDA | MISHAHARA | 33,403,813,000 | 39,071,597,000 | 5,667,784,000 | 17 |
| | OC | 28,065,472,000 | 28,065,472,000 | 0 | 0 |
| MAENDELEO | NDANI | 458,190,778,000 | 458,190,788,000 | 0 | 0 |
| **JUMLA BAJETI** | **JUMLA KUU** | **519,660,073,000** | **525,327,857,000** | **5,667,784,000** | **1.09** |

**Chanzo:** *Randama ya Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo kuhusu Mwelekeo wa Bajeti kwa Mwaka 2026/2027*

**Chati Na. 4: Ulinganisho wa Bajeti 2025/2026 na 2026/2027 (Fungu 96)**




**Chanzo:** *Usanifu wa Kamati kutoka kwenye Taarifa za Randama ya Wizara kwa Mwaka 2026/2027*

### 2.3.3 Makadirio ya Matumizi ya Kawaida

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilichambua makadirio ya bajeti ya matumizi ya kawaida kwa mwaka wa fedha 2026/2027 kwa

kulinganisha na mwaka wa fedha 2025/2026. Matokeo ya uchambuzi yameonesha mambo yafuatayo:-

(i) Makadirio ya matumizi ya kawaida yameongezeka kwa **asilimia 14.82** ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2025/2026;

(ii) Ongezeko la Bajeti ya mishahara kwa Wizara hii limeongezeka kwa **asilimia 17** ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2025/2026;

(iii) Bajeti ya matumizi ya uendeshaji yaani matumizi mengineyo haijaongezeka ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2025/2026;

(iv) Bajeti ya matumizi mengineyo kwa mwaka 2026/2027 ni sawa na **asilimia 5.34** ya jumla ya bajeti ya Wizara hii. Uwiano huo unatofautiana na mwaka wa fedha 2025/2026, ambapo bajeti ya matumizi mengineyo ni **asilimia 5.4** ya jumla ya bajeti ya Wizara.

## 2.4 Majumuisho ya Sehemu ya Pili

**Mheshimiwa Spika**, sehemu hii imefafanua uchambuzi wa taarifa ya utekelezaji kwa mwaka wa fedha 2025/2026 na kuonesha makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka 2026/2027. Mambo makuu matatu yamejitokeza kama ifuatavyo:

(i) Upangaji wa lengo la makusanyo umebainika kuhitaji tathmini kwa kutumia uzoefu uliopatikana kwa mwaka wa fedha 2025/2026;

(ii) Utekelezaji wa kazi zilizopangwa na Wizara ulizingatia majukumu ya msingi ya Wizara na uliendana na upatikanaji wa fedha kwa mwaka wa fedha 2025/2026;

(iii) Makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2026/2027 yanawezesha Wizara hii kuendelea na utekelezaji wa majukumu yake; na

(iv) Mipango ya Wizara na vipaumbele kwa mwaka wa fedha 2026/2027 imezingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 na Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2025/2030.

## SEHEMU YA TATU

## 3.0 MAONI, USHAURI NA HITIMISHO

### 3.1 Maoni

**Mheshimiwa Spika**, baada ya uchambuzi, naomba kutoa maoni ya Kamati kwa kuzingatia matokeo ya uchambuzi. Maoni haya yanajenga msingi wa ushauri nitakaoutoa. Maoni hayo ni kama ifuatavyo:-

(i) Kutokupatikana kwa fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya Mradi wa Ujenzi na Ununuzi wa Mitambo ya Kisasa ya Uchapaji *(TSN)* ni jambo linaloweza kuathiri ukamilishaji wa mradi huo na pengine kusababisha hasara kwa Serikali.

(ii) Kuendelea kutenga bajeti na kutoa fedha kwa wakati kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa viwanja vitatu (3) vya mazoezi katika Mkoa wa Dar es Salaam na viwanja vitano (5) vilivyopo mkoani Arusha ni jambo linaloweza kufanikisha maandalizi madhubuti ya AFCON 2027. Aidha, pamoja na kutumika wakati wa Mashindano ya Mpira wa Miguu kwa timu za Taifa za Wanaume Afrika (AFCON 2027), vitasaidia kupunguza utegemezi wa Uwanja wa Benjamin Mkapa.

(iii) Kupungua kwa wigo wa ukusanyaji wa Mapato ya Tozo kwa Bodi ya Filamu Tanzania kunakosababishwa na kupungua kwa idadi ya waandaji wa filamu kutokana na mabadiliko ya soko la filamu pamoja na kukua kwa

teknolojia kunadhoofisha ukusanyaji wa maduhuli kwa taasisi hiyo.

(iv) Ufinyu wa bajeti kwa ajili ya ujenzi wa Arena ya Sanaa na Michezo unakwamisha uwezekano wa kuongeza fursa za ajira, kukuza uchumi, kuitangaza Tanzania kimataifa, kukuza vipaji vya vijana, kuimarisha umoja na kuboresha afya.

(v) Kutokuwepo kwa mpango wa Wizara kukamilisha mchakato wa vazi la Taifa kunafifisha azma ya Serikali kuweka utambulisho wa Taifa kupitia mavazi.

(vi) Kutokukamilika kwa ujenzi wa miundombinu ya barabara zinazoelekea ndani na nje ya Uwanja wa Arusha kutaathiri mwenendo mzima na uchelewashaji wa maandalizi ya Mashindano ya AFCON 2027.

### 3.2 Ushauri

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na maoni yalivyoelezwa hapo juu, Kamati ilizingatia ipasavyo maoni hayo na kuyatumia kama msingi wa ushauri ufuatao:-

(i) Serikali iendelee kutoa fedha za Mradi wa Ujenzi na Ununuzi wa Mitambo ya Kisasa ya Uchapaji *(TSN)* kwa kiwango kilichokusudiwa ili kukamilisha mradi huo kwa wakati na kuipunguzia hasara zinazoweza kuzuilika.

(ii) Serikali ikamilishe ujenzi wa viwanja vitatu (3) vya mazoezi katika Mkoa wa Dar es Salaam na viwanja vitano (5) vilivyopo mkoani Arusha kwa wakati ili Tanzania iweze kukidhi vigezo vya kuandaa Mashindano ya Mpira wa Miguu kwa timu za Taifa za Wanaume Afrika (AFCON 2027).

(iii) Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo iboreshe na kuongeza wigo wa ukusanyaji wa mapato ya Bodi ya Filamu Tanzania kwa kuendana na maendeleo ya dunia, kurahisisha mawasiliano, kuboresha ubunifu na kuongeza ufanisi katika uzalishaji na usambazaji wa taarifa na kazi za wasanii.

(iv) Serikali iongeze bajeti kwa ajili ya ujenzi wa Arena ya sanaa na michezo kwa kuwa kukamilika kwa utekelezaji wa mradi huu kutaongeza fursa za ajira, kukuza uchumi, kuitangaza Tanzania kimataifa, kukuza vipaji vya vijana, kuimarisha umoja na kuboresha afya. Ushauri huu unaendana na mwelekeo alioutoa Mheshimiwa Rais wakati wa Hotuba yake akilizindua Bunge la 13:

**Nanukuu,** *"Tunaendelea na maandalizi ya ujenzi wa studio ya kisasa ya filamu ili kupandisha thamani ya kazi za wacheza filamu wetu hapa nchini. Tutajenga ukumbi wa kisasa wa maonyesho ili kuwawezesha wasanii wetu kufanya matamasha ya kimataifa, na kuvutia wasanii wa nje wakubwa kufanya matamasha nchini. Tunataka*

*sanaa, filamu na muziki zitengeneze ajira na kuchangia uchumi wa Taifa." (uk.22-23)* **mwisho wa kunukuu.**

(v) Serikali ifufue na kukamilisha mchakato wa upatikanaji wa vazi la Taifa ili kuimarisha utambulisho wa Taifa, kukuza umoja wa kitaifa, kukuza uchumi, ajira pamoja na kuhifadhi na kuendeleza utamaduni wa Mtanzania.

(vi) Serikali iongeze kasi ya ujenzi wa miundombinu ya barabara za ndani na nje ya Uwanja wa Arusha ili kukamilisha maandalizi ya Mashindano ya AFCON 2027.

## 3.3 Hitimisho

**Mheshimiwa Spika**, nachukua fursa hii kukushukuru kwa kunipa nafasi kwa ajili ya kuwasilisha Taarifa hii. Aidha, nawashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo ambao maoni, ushauri na ushirikiano wao umewezesha kukamilika kwa taarifa hii. Naomba majina yao kama yalivyoorodheshwa katika Taarifa hii yaingie kwenye Taarifa Rasmi za Bunge *(Hansard)*:-

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Mhe. Husna Juma Sekiboko, Mb | - | Mwenyekiti |
| 2. | Mhe. Cornel Lucas Magembe, Mb | - | M/Mwenyekiti |
| 3. | Mhe. Hamis Shabani Taletale, Mb | - | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Asha Ramadhan Baraka, Mb | - | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Asha Juma Feruzi, Mb | - | Mjumbe |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 6. | Mhe. Regina Henry Mikenze, Mb | - | Mjumbe |
| 7. | Mhe. Asha Juma Kombo, Mb | - | Mjumbe |
| 8. | Mhe. Dkt. Christine Christopher Mnzava, Mb | - | Mjumbe |
| 9. | Mhe. Yumna Mmanga Omar, Mb | - | Mjumbe |
| 10. | Mhe. Kijakazi Yunus Mohamed, Mb | - | Mjumbe |
| 11. | Mhe. Mohamed Abdulla Makame, Mb | - | Mjumbe |
| 12. | Mhe. Mabula Johnson Magangila, Mb | - | Mjumbe |
| 13. | Mhe. Fagason Aron Nkingwa, Mb | - | Mjumbe |
| 14. | Mhe. Juma Abdalla Juma, Mb | - | Mjumbe |
| 15. | Mhe. Bakari Shingo Bakari, Mb | - | Mjumbe |
| 16. | Mhe. Onesmo Merdson Mnkondya, Mb | - | Mjumbe |
| 17. | Mhe. Baraka Ulimboka Mwamengo, Mb | - | Mjumbe |
| 18. | Mhe. Isaya Moses Mngurumi, Mb | - | Mjumbe |
| 19. | Mhe. Dkt. Mashaka Doto Biteko, Mb | - | Mjumbe |
| 20. | Mhe. Kassim Amar Mbaraka, Mb | - | Mjumbe |

**Mheshimiwa Spika,** kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati napenda kumshukuru – Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo Mhe. Paul Christian Makonda (Mb), Naibu Waziri - Mhe. Hamis Mohamed Mwinjuma (Mb), Katibu Mkuu wa Wizara hii Ndg. Gerson Partinus Msigwa, Naibu Katibu Mkuu Ndg. Methusela Stephen Ntonda, pamoja na Watendaji wengine wa Wizara kwa ushirikiano mkubwa walioipa Kamati katika kutekeleza majukumu yake na kwa usimamizi mzuri wa majukumu ya Wizara kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya kipekee napenda kuwashukuru watumishi wote wa Ofisi ya Bunge wakiongozwa na Katibu wa Bunge *Ndg. Baraka Ildephonce Leonard,* kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake vema katika wakati wote ilipokutana na hata wakati wa utayarishaji wa taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu lipokee Taarifa hii ili lijadili na likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 kama yalivyowasilishwa na Mtoa Hoja.

**Mheshimiwa Spika**, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha.

Husna Juma Sekiboko, Mb
**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ELIMU, UTAMADUNI NA MICHEZO**

04 Mei, 2026

# VIAMBATISHO

## KIAMBATISHO NA 1

### YATOKANAYO NA MIRADI YA MAENDELEO ILIYOKAGULIWA

**Mheshimiwa Spika**, Wakati wa ziara za ukaguzi wa miradi inayotekelezwa na Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Kamati ilipokea taarifa za utekelezaji wa miradi na kuona hali halisi kwenye maeneo ya utekelezaji wa miradi husika. Uchambuzi wa taarifa hizo ulilinganishwa na hali halisi ya hatua zilizofikiwa pamoja na madhumuni ya kutekelezwa kwa miradi inayohusika. Naomba kutoa taarifa kuhusu matokeo ya ukaguzi na uchambuzi wake kama ifuatavyo:

**a) Mradi Na. 6586 wa Ujenzi wa Uwanja wa Mpira wa Miguu Arusha**

**Mheshimiwa Spika,** Mradi huu unahusu ujenzi wa Uwanja wa Mpira wa Miguu Jiji la Arusha. Taarifa zinaonyesha kuwa, fedha zinazotumika kutekeleza mradi huu ni fedha za ndani kwa asilimia **100**. Aidha, jumla ya gharama ya mradi wote ni **Shilingi 338,542,000,000.**

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2025/2026 mradi ulitengewa jumla ya shilingi **193,096,682,000** kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu. Kamati ilijulishwa kuwa, hadi kufikia Februari, 2026 mradi ulipokea **Shilingi 106,742,579,088** sawa na **asilimia 55.2**. Aidha, mradi umefikia asilimia 75 ya utekelezaji kazi zilizofanyika ni

pamoja na ujenzi wa majukwaa ya zege, vyumba mbalimbali katika sehemu zote za uwanja (asilimia 96), kupiga lipu sehemu mbalimbali za uwanja (asilimia 85), usawazishaji wa majukwaa ya kukaa watazamaji kwa ajili ya kufunga viti (asilimia 82) ujenzi wa paa la uwanja (asilimia 60) uwekaji mifumo mbalimbali ya kihandisi kama vile mifumo ya zimamoto, umeme, majisafi na majitaka, viyoyozi, *CCTV camera* na TEHAMA (asilimia 58, umaliziaji wa sehemu mbalimbali za ndani kama vile kuweka terrazzo, marumaru, vioo, dari (asilimia 54) ujenzi wa sehemu ya kuchezea wachezaji – pitch (asilimia 52) na kazi za usawazishaji wa sehemu ya nje – *lands caping* (asilimia 23).

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kwa utekelezaji mzuri wa mradi huu kwani kukamilika kwa mradi huu kutatoa fursa mbalimbali kwa jamii ikiwemo ajira kwa vijana, kuinua vipaji vya michezo na kuchochea shughuli za utalii na hivyo kuinua uchumi wa nchi. Aidha, yapo baadhi ya maeneo yanayohitaji kuwekewa nguvu zaidi hususan ujenzi wa viwanja viwili vya mazoezi na ujenzi wa sehemu ya kuchezea wachezaji *(pitch)* ambapo kwa sasa upo asilimia 52. Ni maoni ya Kamati kwamba, kasi ya ujenzi wa viwanja hivyo iongezeke ili vikamilike kwa wakati.

**b) Mradi Na. 6523 Ukarabati wa Eneo Changamani la Michezo la Uwanja wa Benjamin Mkapa na Uhuru (Dar es Salaam)**

**Mheshimiwa Spika,** Mradi wa ukarabati wa eneo changamani la michezo la Uwanja wa Benjamin Mkapa na Uhuru unatekelezwa kwa gharama ya **shilingi 41,713,423,339.93.** Katika mwaka wa fedha 2025/2026 mradi ulitengewa kiasi cha **shilingi 19,908,288,818.72.** Hadi kufikia Februari 2026 mradi umepokea jumla ya **shilingi 9,038,058,363.12** sawa na **asilimia 45.40**. Aidha, shughuli zilizotekelezwa katika uwanja wa Benjamin Mkapa ni pamoja na ukarabati wa vyumba vya kubadilishia nguo wachezaji (asilimia 97), chumba na maeneo ya waandishi wa habari (asilimia 100), viti 60,000 vya watazamaji vya uwanjani (asilimia 90), ubao mkubwa wa matangazo (asilimia 100), eneo la watu mashuhuri (asilimia 100), lifti (asilimia 100), mifumo ya TEHAMA (asilimia 98).

Vilevile, ukarabati wa mifumo ya vyoo (asilimia 100), eneo la kukimbilia riadha (asilimia 100), mfumo wa viyoyozi (asilimia 98), chumba cha kupambana na dawa na mbinu haramu michezoni (asilimia 100), mfumo wa umeme (asilimia 97), kupaka rangi maeneo mbalimbali ya uwanja (asilimia 96), kufanya ukarabati wa dari katika jengo zima la uwanja (asilimia 98), kubadilisha taa 352 (asilimia 100),

kuondoa milango ya zamani na kuweka mipya (asilimia 85) na mifumo ya kudhibiti moto (asilimia 90).

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilibaini kuwa kuwepo kwa matumizi ya uwanja wakati shughuli za ukarabati zinaendelea kunaathiri mwenendo mzima wa ukarabati ikiwemo kuathiri ratiba ya mkandarasi na kuharibu miundombinu inayokamilika. Vilevile, Kamati ilibaini changamoto ya mkandarasi kuchelewa kumaliza kazi katika muda wa mkataba hivyo kuathiri mwenendo mzima wa ukamilishaji wa mradi na shughuli za matumizi ya uwanja.

**Mheshimiwa Spika,** mradi wa ukarabati wa Uwanja wa Uhuru Dar es Salaam ulikadiriwa kugharimu jumla ya **shilingi 22,329,870,148.26.** Mwaka 2025/2026 mradi ulitengewa **shilingi 10,000,000,000** ambapo hadi kufikia Februari 2026, mradi umepokea jumla ya **shilingi 8,216,120,983.49** sawa na **asilimia 82.16.** Kamati imebaini miongoni mwa kazi zilizofanyika ni pamoja na ukarabati katika vyumba vya kubadilishia nguo wachezaji (asilimia 50), kuezeka paa la jukwaa kuu na watazamaji (asilimia 100), kufunga viti vipya uwanjani (asilimia 30), kukarabati eneo la watu mashuhuri (asilimia 80), mifumo ya vyoo (asilimia 90), eneo la kuchezea mpira (asilimia 75), eneo la kukimbia riadha (asilimia 70), mfumo wa viyoyozi (asilimia 5), kusakinisha taa

za uwanja (asilimia 40) na kukarabati mfumo wa umeme (asilimia 50).

**Mheshimiwa Spika,** kimsingi Kamati imebaini kuwa ukarabati katika Uwanja wa Uhuru upo katika hatua nzuri pamoja na kwamba yapo baadhi ya maeneo yanahitaji kuongezewa nguvu zaidi hususan mfumo wa viyoyozi (asilimia 5), na ufungaji wa viti vipya uwanjani (asilimia 30). Ni rai ya Kamati kuwa kasi ya ukarabati iongezwe ili mradi ukamilike kwa wakati.

**c) Mradi Na. 6505, Ujenzi na Ununuzi wa Mitambo ya Uchapaji wa Magazeti ya Serikali**

**Mheshimiwa Spika;** Mradi huu kwa ujumla wake umekadiriwa kugharimu jumla ya **Shilingi Bilioni 32.1** hadi kukamilika kwake. Katika Mwaka wa Fedha 2025/2026 mradi huu uliidhinishiwa kiasi cha **Shilingi 11,000,000,000.00** ikijumuisha ujenzi wa jengo la kusimika mitambo ya uchapishaji na ununuzi wa mitambo ya uchapishaji. Hadi kufikia mwezi Februari, 2025 kiasi cha **Shilingi 4,191,563,062.07** kilichotengwa kilikuwa kimepokelewa sawa na **asilimia 38.11**.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilibaini kuwa kuna mtiririko mdogo wa fedha zinazotolewa hali inayopelekea kusuasua kwa utekelezaji wa mradi huu na kuongezeka kwa gharama za mradi kutokana na kuchelewa kwa

fedha za malipo ya wazabuni na wakandarasi ukilinganisha na matakwa ya kimkataba. Ni rai ya Kamati kuwa Fedha zote zilizoidhinishwa na Bunge lako tukufu zitolewe zote na kwa wakati ili mradi huu uanze kufanya kazi na kuleta tija kwa Taifa.

**KIAMBATISHO NA 2**

## UTEKELEZAJI WA MAONI NA USHAURI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ELIMU, UTAMADUNI NA MICHEZO

Wakati wa kuchambua Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Kamati ilishauri masuala mbalimbali ambapo maelezo ya Wizara kuhusu utekelezaji wa maoni na ushauri huo ni kama ifuatavyo:-

| Na. | Maoni na Ushauri | Utekelezaji |
|---|---|---|
| 1. | Serikali iendelee kutoa fedha za miradi ya maendeleo kwa wakati na kwa kiwango kilichokusudiwa ili kukidhi matarajio kwa Wizara. | Katika mwaka wa Fedha 2024/25, Wizara iliidhinishiwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania jumla ya shilingi 258,190,788,000 kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Wizara ikiwa katika utekelezaji wa bajeti yake iliyokuwa imepitishiwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ilipofika tarehe 08 Desemba, 2024 Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliihamisha Idara ya Habari-MAELEZO kutoka iliyokuwa Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari na kuipeleka katika Wizara iliyokuwa ya Utamaduni, Sanaa na Michezo na kuunda Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo. Kutokana na mabadiliko hayo pamoja na sababu nyingine ikiwemo kuratibu mashindano ya CHAN 2024 yalisababisha mabadiliko katika bajeti, ambapo bajeti ya miradi ya maendeleo iliongezeka hadi kufikia Shilingi 305,521,486,465.36 kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Katika kipindi cha Julai 2024 hadi Juni 2025, Wizara ilipokea jumla ya shilingi 265,342,284,774.94 kwa ajili ya miradi ya |

| Na. | Maoni na Ushauri | Utekelezaji |
|---|---|---|
| | | maendeleo sawa na asilimia 86.85 ya bajeti iliyoidhinishwa. Katika mwaka wa fedha 2025/26, Wizara imeidhinishiwa jumla ya shilingi 458,190,788,000.00 kwa ajili ya miradi ya maendeleo, ambapo katika kipindi cha Julai 2025 hadi Februari 2026, Wizara imepokea kiasi cha Shilingi 289,878,498,984.34 kwa ajili ya miradi ya maendeleo sawa na asilimia 63.3 ya bajeti iliyoidhinishwa. |
| 2. | Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo iandae mikakati ya kuboresha viwanja vingine vyenye hadhi ya kuendesha mashindano ya kitaifa na kimataifa ili kupunguza mfululizo wa matumizi ya Uwanja wa Benjamin Mkapa. | Wizara imeendelea na ukarabati na ujenzi wa viwanja vipya vya michezo ili kupunguza matumizi ya mfululizo ya uwanja wa Benjamin Mkapa. Viwanja vilivyokarabatiwa ili kukidhi vigezo ni uwanja wa Uhuru, Meja Jen. Isamuhyo, Gymkana na uwanja wa shule ya Sheria (Law school). Aidha, viwanja vinavyojengwa ni uwanja wa Arusha na Dodoma vyenye uwezo wa kuchukua watazamaji 32,000 na vituo vya mazoezi na kupumzikia wananchi vya Dar es Salaam na Dodoma vyenye viwanja vinne (4) vya mpira wa miguu pamoja na Akademia ya Michezo yenye viwanja vitatu (3) inayojengwa Malya, mkoani Mwanza.<br><br>Vile vile, Serikali imeanza ujenzi wa viwanja vitatu (3) vya Farasi, Gymkana Annex na Leaders Club. Katika hatua nyingine, Serikali inajenga viwanja vitano (5) vya mazoezi jijini Arusha katika eneo la Magereza Kisongo, Uwanja wa Mgambo, eneo la Police Field Force na Engutoto. Viwanja hivi pamoja na kutumika wakati wa AFCON 2027 vitasaidia kupunguza utegemezi wa uwanja wa Benjamin Mkapa. |
| 3. | Serikali iendelee kutenga bajeti kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa Uwanja wa Arusha ili kufanikisha na kukamilisha | Serikali inaendelea na ujenzi wa uwanja mpya wa michezo jijini Arusha chini ya Mkandarasi China Railway Construction Engineering Group Co. Ltd (CRCEG) na Mshauri Elekezi Dar |

| Na. | Maoni na Ushauri | Utekelezaji |
|---|---|---|
| | utekelezaji wa mradi huu kama ilivyokusudiwa na pia kuongeza chachu ya utalii na kuwa kituo muhimu katika Mashindano ya Mataifa ya Afrika (AFCON) | Alhandasah Consultants (Chair&Partners) E.C. Limited. Gharama ya mradi ni shilingi 347,307,644,000 (ikijumuisha VAT) na unatarajiwa kuwa na uwezo wa kuhudumia watazamaji 32,000.<br><br>Katika mwaka wa fedha 2024/25, Serikali ilitenga na kutoa kiasi cha shilingi 153,161,763,553.50 kwa ajili ya ujenzi wa uwanja wa Arusha. Serikali katika kuhakikisha inakamilisha maandalizi ya kuwa mwenyeji wa mashindano ya AFCON 2027 kwa kushirikiana na nchi za Kenya na Uganda, kwa mwaka wa fedha 2025/26, imetenga shilingi 162,976,682,000.00 kwa ajili ya mradi wa ujenzi wa uwanja wa Arusha. Hadi Februari 2026, Serikali imetoa shilingi 106,742,579,088 sawa na asilimia 65.5 ya bajeti iliyotengwa. Kwa ujumla, hadi Februari 2026 ujenzi wa uwanja umefikia asilimia 75 na jumla ya shilingi 256,208,264,022.55 zimetolewa, sawa na asilimia 73.8 ya gharama ya mradi. |
| 4. | Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo iboreshe na kuongeza wigo wa ukusanyaji wa Mapato ya Tozo za Hakimiliki kwa kuongeza vifaa vinavyotozwa Tozo hii hasa vya Kidijitali. | Wizara kupitia COSOTA imeandaa andiko la kuongeza vifaa 25 vinavyotozwa tozo ya hakimiliki ambapo vitafikia jumla ya vifaa 38 kutoka vifaa 13 vinavyotozwa hivi sasa. Aidha, andiko limependekeza kiwango cha tozo kinachotozwa kutoka asilimia 1.5 na kuwa asilimia 5 hadi 10 ili kuendana na mikataba ya kikanda inayoelekeza nchi wanachama kutoza kiwango cha kati ya asilimia 5 hadi 15. Vilevile, ili kurahisisha kuongeza vifaa zaidi kutokana na mabadiliko ya sayansi na teknolojia, imependekezwa mabadiliko ya kifungu cha 53 cha Sheria ya Hakimiliki na Hakishiriki, Na. 7 ya Mwaka 1999 kwa kumpa mamlaka Waziri mwenye dhamana uwezo wa kuongeza au kupunguza vifaa vinavyotozwa pamoja na |

| Na. | Maoni na Ushauri | Utekelezaji |
|---|---|---|
| | | kiwango cha tozo. Suala hili linaendelea katika ngazi za majadiliano ndani ya Serikali kwa ajili ya uamuzi wa utekelezaji ambapo kikosi kazi maalum cha Wizara ya Fedha pamoja na wadau mbalimbali wameshapitia maandiko ya mapendekezo yanayohusiana na marekebisho ya sheria ya fedha ikiwemo Andiko la kuongeza vifaa 25 vinavyoombwa kutozwa tozo ya hakimiliki. |
| 5. | Fedha zote zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya ujenzi na ununuzi wa mitambo ya uchapaji zitolewe kabla ya tarehe 01 Julai, 2025 | Katika mwaka wa fedha 2024/25, Wizara iliidhinishiwa jumla ya shilingi 3,517,160,000 kwa ajili ya ujenzi na ununuzi wa mitambo ya uchapaji. Hadi tarehe 30 Juni, 2025 kiasi cha shilingi 2,440,617,727.64 kilipokelewa sawa na asilimia 69 ya bajeti iliyotengwa. Kwa mwaka wa fedha 2025/26, Wizara iliidhinishiwa jumla ya shilingi 14,000,000,000 ambapo hadi kufikia Februari 2026, Wizara imepokea kiasi cha shilingi 4,191,563,062, sawa na asilimia 30 ya bajeti iliyotengwa. Utekelezaji wa mradi unaendelea ambapo hatua iliyofikiwa ni asilimia 66.04 kwa upande wa ujenzi wa kiwanda cha uchapaji na asilimia 85.20 kwa upande wa ununuzi wa mitambo ya kisasa ya uchapaji. |
| 6. | Serikali ifanye tathmini, utafiti kupitia Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kuhusu utendaji kazi wa TSN ili kuweza kujua ni sababu zipi zimesababisha jengo la kiwanda cha uchapaji kutokukamilika kwa wakati. | Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) imefanya tathmini ya utekelezaji wa mradi namba 6505 wakati wa ukaguzi wa hesabu za Kampuni kwa mwaka wa fedha 2024/25. Tathmini imebaini uwepo wa changamoto ya upungufu wa rasilimali fedha kwa ajili ya malipo ya mkandarasi na ununuzi wa mitambo mipya ya kisasa ya uchapaji. Katika jitihada za kuhakikisha utekelezaji wa mradi unaendelea kwa kuhakikisha upatikanaji wa fedha na ukamilishaji wa ujenzi. Hatua zifuatazo zilichukulia: |

| Na. | Maoni na Ushauri | Utekelezaji |
|---|---|---|
| | | i. Tarehe 17 Julai, 2024 Serikali iliitisha kikao na Mwenyekiti wa Makampuni ya Group Six International Limited kuhusu kuendelea na ujenzi wakati taratibu za malipo zinaendelea kufanyika;<br>ii. Tarehe 23 Oktoba, 2025 kilifanyika kikao kati ya Bodi ya TSN na Mwenyekiti wa Makampuni ya Group Six International Limited, kujadilianakuhusu ukamilishaji wa ujenzi wa Mradi Na. 6505;<br>iii. Katika mwaka wa fedha 2024/25, Wizara iliidhinishiwa jumla ya shilingi 3,517,160,000 kwa ajili ya ujenzi na ununuzi wa mitambo ya uchapaji. Hadi tarehe 30 Juni, 2025 kiasi cha shilingi 2,440,617,727.64 kilipokelewa sawa na asilimia 69 ya bajeti iliyotengwa; na<br>iv. Kwa mwaka wa fedha 2025/2026 hadi kufikia Februari 2026 kiasi cha Shilingi 4,191,563,062 kimepokelewa kwa ajili ya utekelezaji wa mradi. |
| 7. | Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo ikamilishe ujenzi wa Jengo la Kiwanda cha Uchapaji ili kupunguza gharama za uendeshaji na utunzaji wa mitambo katika maghala ya Taasisi nyingine. | Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2024/25, Wizara ilipokea shilingi 2,440,617,727.64 kwa ajili ya utekelezaji wa mradi. Aidha, katika mwaka wa fedha 2025/26, Serikali imetenga Shilingi 14,000,000,000 kwa ajili ya kukamilisha utekelezaji wa mradi, ambapo hadi Februari 2026 kiasi cha Shilingi 4,191,563,062 kimepokelewa na kutumika.<br><br>Ujenzi wa jengo la kiwanda cha uchapaji umefikia asilimia 66 na ununuzi wa Mitambo mipya ya kisasa imefikia asilimia 85. Serikali itaendelea kutoa kipaumbele kwa mradi huu ili ukamilike kwa wakati na kuanza uzalishaji kwa lengo la kufikia manufaa tarajiwa. |